# WATEULE WENGI WANAKUFA MAPEMA AU WANAPITIA KATIKA MATESO MENGI YASIYO NA SABABU KWA SABABU YA KUWAPA MBWA SIRI ZAO WALIZOPEWA NA KRISTO

# MAANDIKO: MATH. 7:6, WAAMUZI 16:4-5.

1. **UTANGULIZI**

   Mpango wa Mungu tangu mwanzo wa kuumbwa kwa Adamu wa kwanza ni kuweka siri (mambo) yake ya ajabu na ya pekee sana kwa mwanadamu ili Mwanadamu aweze kuwa wakili wake hapa duniani. ***1Kor.4: 1-2, Zab. 25:14, Mwanz. 2:15-17.***

- **Siri ni jambo linalofichwa kwa watu wengi na wanajulishwa wateule wachache ambao wana uwezo wa kulitunza jambo hilo ndani ya mioyo yao (usalama wa Taifa).**

  **Note:** Mungu tangu mwanzo ni Mungu wa siri kwa maana anajua faida ya kuficha siri katika baadhi ya mambo kwa watu wote na kuyafunua kwa watu wachache tu ambao anafahamu kwamba wanao uwezo wa kuyatunza mioyoni mwao hadi wakati wa kufaa ufike. Ni jambo moja tu kubwa ambalo mpaka leo amelitunza yeye mwenyewe na hajawahi kumwambia mtu yeyote maana anawafahamu wanadamu jinsi walivyo na madhara ambayo yangetokea iwapo jambo hilo angelimwambia mtu. ***Math. 24:36*** **"swala la kurudi kwa Yesu mara ya pili ili kulichukua Kanisa!! Mungu hajamwambia kabisa binadamu yeyote, ametaja dalili za kurudi kwake tu**

2. **Ni kwa nini hasa Mungu anawapa wateule wake siri zake na kisha kuwapa masharti ya kutowaambia watu wengine?? Math. 17:1-9.** Sababu kubwa ni kwa ajili ya **usalama** wao na pia kwa ajili ya usalama wa kundi walilokabidhiwa kuliongoza ili baadaye waweze kupata mafanikio yatakayoshangaza wale wote ambao hawakutegemea kuona tunafanikiwa kwa kiasi hicho.

**Mfano.** Kama Bwana Yesu asingewakataza Petro, Yohana na Yakobo wasitoe siri ya kile walichokiona mlimani wakati Yesu alipogeuka sura yake mbele yao; mambo matatu au manne au hata matano yangetokea kwao tangu wakati ule.

a. **Kwanza.** Kabisa wangeanza kumtukuza Yesu Kristo hata kabla wakati wake uliokuwa umepangwa na Mungu Baba haujafika. ***Filipi 2:5-11, Efes 1:20-23, Ebr. 1:1-14***.

b. **Pili.** Kungekuwa na mgawanyiko mkubwa kati ya hawa wanafunzi watatu walimwona Yesu hali yake pale mlimani akigeuka sura yake na wale wengine **tisa** ambao aliwaficha hali yake halisi (upinzani ungekuwa mkubwa)

c. **Tatu.** Hawa wanafunzi watatu waliomwona Yesu akigeuka sura yake wangejiona bora kuliko wale tisa na wangetumia hali ile kujaa **kiburi** cha uzima.

d. Shetani angetumia nafasi ile kuwahubiria wale tisa kwamba Yesu hawathamini na ana upendeleo na angefaulu sana kuwafanya wasimwamini tena kama Kiongozi wao anayewatendea wote haki sawa.

e. **Wale tisa** nao wangeanzisha madai kwa Yesu ili abadilike sura wamwone kama alivyojibadilisha na kuonekana kwa wale watatu n.k

3. **Sasa tuone kwa nini Yesu mwenyewe alifundisha somo hili gumu na kutumia maneno mahumu sana!!** ***Math. 7:6***
**"Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua!!**

a) **Samsoni** alikuwa na vitu vitakatifu sana moyoni mwake (Lulu) ambavyo hakutakiwa kumwambia Delila (mbwa). ***Waam. 13:3-4*** na alipotoa siri yake yote mbele ya mbwa ikawa ndiyo mwisho wa usalama wake na maisha yake kwa ujumla na utumishi wake vikaishia hapa. ***Waam. 16:4-5, 6-23, 24-31.***

b) **Mwanzo 37:1-11.** Yusuph alipotoa vitu vitakatifu mno alivyoambiwa na Bwana katika ndoto kwa ndugu zake ndiyo ukawa mwanzo wa chuki kubwa hadi mipango ya kumwua ikapangwa. **Mwanz. 37:15-28.** Kama sio Mungu Baba kuingilia kati kabisa, kweli ndoto zote za Yusufu zilikuwa zinaishia hapa pamoja na maisha yake yote. **Siyo kila mtu aitwaye ndugu anayefurahia Baraka zako unazopewa na Bwana wewe, wengine ni mbwa na nguruwe na ndiyo watakaokurarua hovyo baadaye.**

c) **Mamajusi** (wise men) watu wenye busara (hekima) walipewa neema ya kuiona nyota (kuona kuzaliwa kwa Mfalme Yesu) halafu badala ya kutunza siri hiyo, wao wakaenda kumsumlia Herode!! Kama siyo Mungu kuingilia kati; Yesu angeuawa na mbwa/nguruwe mapema kabla hata ya kuanza kazi ya ukombozi aliyoijia hapa Ulimwenguni. ***Math. 2:1-18.*** **Herode akiwa amejaa wivu alitoa maneno mazuri na laini sana kwa Mamajusi hawa tofauti kabisa na alivyokuwa ndani ya moyo wake.**

**Note: unapoanza tu kutoa siri za Baraka zako hovyo hovyo hadi kwa mbwa na nguruwe, unaalika wewe mwenyewe matatizo pamoja na kifo chako kabla ya wakati wako aliokupangia Mungu. Narudia tena kuwaambia kwamba siyo wote wanaofurahia kuona mafanikio uliyo nayo na wao hawana amani uliyo nayo na ndoa yako na watoto wako na wao hawana; afya uliyo nayo na wao hawana!! Ni kwa vile hatujafunuliwa tu hao mbwa jinsi wanavyopanga kukanyaga Baraka zetu.**

d) **Mwone nabii huyu kijana mskini!!** ***1Wafal. 13:1-30.*** Pale tu alipotoa siri zake mbele ya mbwa; ndiyo ukawa mwanzo wa mbinu za kutafuta kumwangamiza!! Na kama Samsoni alivyoangamizwa kwa urahisi mno kupitia Delila **(Delila alikuwa chotara- Baba Mfilisti na mama Myahudi) na Delila alikulia kwa mama yake na hiyo alikuwa anaongea Kiyahudi fasaha, ndiyo sababu**

**Samsoni alimwaga moyo wake wote akifahamu anaongea na mtu wa kabila lake kumbe ni mbwa!!** Ndivyo na huyu Nabii kijana alivyojimwaga kwa huyu Nabii mzee akijua kwamba ana mshirikisha Mtumishi mwenzie kumbe anamshirikisha mbwa!!

e) **Elisha Nabii** alikuwa sababu ya Taifa la Israel kuwa salama katika kipindi chake kwa sababu Elisha hakuwa mtumishi wa kuropoka ropoka mbele ya mbwa kuhusiana na siri ambazo Mungu ameweka ndani yake. ***2Wafal. 6:8-23.***

f) **Rahabu kahaba** alipona kwa sababu moja tu kubwa, alitunza siri ya wale wapelelezi waliotumwa na Yoshua. ***Yosh. 2:17-21, 6:21-27.***

g) **Salama ya mtumishi wa Mungu Paulo** ilitegemea wakati Fulani moyo wa mjomba wake pamoja na jemadari wa kikosi cha jeshi waliotunza siri baada ya kufahamu kwamba kuna watu wapatao 40 ambao wamepatana kutokula wala kunywa hadi watakapomwuua Paulo. ***Mdo. 23:12-35.***

**Note: Taifa letu linaendelea kuwa salama kutokana tu na watu walioaminiwa kutunza usalama kuwa waaminifu pamoja na kutunza siri za nchi.**

4. **Mara nyingi siri za Mungu tunapewa wakati tunapokuwa tumezama kwa kina katika maombi na kuruhusu Roho Mtakatifu aombe kwa kuugua sana ndani yetu. 1Kor. 14:2, Amosi 3:7.**

**Note:** Zinakuwepo siri nyingine Bwana anakwambia uwaambie watu. ***Kut. 11:1-8.*** Na zinaposemwa kwa wakati sahihi zinakuwa Baraka sana. ***Mith. 15:23, Mith 25:11***

- Mimi naamini kwamba Malkia Esta alipokuwa katika maombi ya kuugua ya siku tatu bila kula wala kunywa, ndipo Mungu alipompa siri zote za jinsi ya kufanya mbele ya mume wake (Mfalme katili sana Ahasuero na mwishoni ndipo; ile siri na jinsi

Malkia Esta alivyofanya ilikuwa ni hekima ya hali ya juu sana na akatoboa siri ya moyo wake baadaye na alifanikiwa sana. ***Est. 3:8-15, 4:16-17, 5:1-8, 9-14, 6:1-14, Est. 7:1-10, 8:1-17*** **Haleluya**.

- Ndivyo ilivyokuwa inatokea hata kwa Daniel na wenzake, walipokuwa katika maombi ya kina na kuzama sana ndipo Mungu Baba alipokuwa anawajuisha siri za ajabu ambazo ndizo ziliwafanya wawe salama wakati wote ***Dan. 2:1-49 (*17-24) 4:1-37 (*17-28).***

  **Mwisho**. Moyo wa Binadamu umetunza siri nyingi mno, nyingine mbaya zitakazoleta madhara baadaye na nyingine nzuri. Roho Mtakatifu tu akipewa nafasi ya kutosha kwa njia ya maombi ya kuugua, atatufunulia siri za Mungu zenye manufaa na usalama wetu ***(1Kor. 2:10-16, 1Kor. 14:4)*** **Ampl Bible says "He who speaks in a tongue edifies and improve himself** (**yeye anenaye kwa lugha nyingine hujiadibisha (hujirekebisha) kimaadili na kujiboresha mwenyewe**. Ee Mungu uwe tayari kutuamini na utujulishe siri zako muhimu katika safari yetu hii ili tufike juu salama. **Amina.**

***Na***
***Ask Dr. L. Mwizarubi***
***20/11/2022.***